

## DHAMBI ISIYOWEZA KUSAMEHEKA?

(MAHUBIRI YA HADHARA OLDONYOWASI – ARUSHA | DEC 16 – 30, 2017)

### Na Almedad Amos

Somo la leo linaohusika na maisha ya mtu binafsi. Tunajua wazi kuwa tunatenda dhambi lakini, Je, ipo dhambi isiyoweza kusameheka? Unawezaje kujua umetenda dhambi isiyoweza kusameheka? Unaweza kuitambua wakati utakapokuwa umefika? Tuna muda kiasi gani wa kujiandaa kabla ya kuingia mbingunii?

Majibu: Wengine watakuwa na muda mpaka wanakufa. Wengine wataufupisha muda wao wa kujiandaa, kwa kutenda dhambi isiyosameheka. Hofu huijaza mioyo yetu hasa pale tunapowaza juu ya dhambi flani ambayo tunadhani haiwezi kamwe ikasameheka. Ni dhambi gani hii ya kutisha ambayo Mungu hawezi kuisamehe? Wengi hudhani kufanya mauaji, kujiua, kuu kutoa mimba au jambo jingine flani la kutisha, au kufanya uzinzi. Je, Biblia inahitaji dhambi ipi hasa kama dhambi isiyosameheka?

Biblia inasema kwamba Mariam Magdalena alifanya dhambi ya uzinzi mara saba, na pia alikuwa na pepo wachafu; lakini alipokiri dhambi zake, Mungu alimsamehe. Kwa hiyo tunatilia mashaka kwamba isiyosameheka si uuaji, uzinzi au hata kujiua wakati mwingine.

Sasa dhambi isiyosameheka ni ipi, kwa mujibu wa Yesu? Katika **Mathayo 12:31 yesu alisema: “Kwa sababu hiyo nawaambia, Kila dhambi na kila neno la kufuru watasamehewa wanadamu, ila kwa kumkufuru Roho hawatasamehewa.”** Ninayo furaha kwa sababu Yesu alisema “kila dhambi inaweza kusamehewa.” lakini hatuwezi kutenda dhambi ya kumkufuru Roho Mtakatifu na bado tukasamehewa. Kwa hiyo kwa mujibu wa Yesu, dhambi isiyosameheka ni dhambi ya kumkufuru Roho Mtakatifu. *Roho Mtakatifu ni nani?*

Kwa mujibu wa Biblia kuna-nafsi tatu alizonazo Mungu, Mungu Baba, Mungu Mwana na Mungu Roho Mtakatifu. Katika **Mwanzo 1:1, 2, 26 tunasoma kwamba zote nafsi tatu zilishiriki katika uumbaji wa ulimwengu huu “hapo mwanzo Mungu aliziumba mbingu nan chi... 2 Roho ya Mungu ikatulia juu ya uso wa maji.... Kisha Mungu akasema, “na tufanye mtu kwa mfano wetu, kwa sura yetu;...”**

Katika **1 Yohana 5:7** Biblia inasema waziwazi na **kwa namna ya kuwatofautisha kwamba wako watatu lakini wote ni mmoja. “8 Kwa maana wako watatu washuhudiaio mbinguni, Baba, na Neno, na Roho Mtakatifu, na watatu hawa ni umoja.”** hapa iko wazi kabisa kwamba Roho wa Mungu ni Moja kati ya Nafsi tatu katika Uungu. Roho Mtakatifu ndiye Mwakilishi wa Yesu hapa duniani.

Biblia inatueleza kwamba hapa duniani kutakua na Roho wa aina mbili, Roho Mtakatifu na Roho Mchafu. We are told in **1 Yohana 4:1: “Wapenzi, msiiamini kila roho, bali zizaribuni hizo roho, kwamba zimetokana na Mungu;**

Watu wengi leo wako katika hatari ya kudanganywa na Roho wa Shetani. Kazi ya Roho Mtrakatifu imeingia katika mkanganyiko, na waliowengi hawaijui, na kazi za Ibilisi zinazofanywa kwa nia ya upotoshaji wakati mwingine imepewa jila la nguvu za Roho wa Mungu. Kuna watu wanasema kumpokea Roho Mtakatifu huambatana na msisimko wa hali ya juu sana, na kupaza sauti zenye makelele mengi na kusema katika lugha ambazo hata msemaji hawezi kuzielewa kwa kuwa ni za kimbungu-mbingu. Lakini nataka kusema sasa na waziwazi kabisa kwamba Roho wa Mungu hatokei namna hiyo katika maisha ya wanadamu.

Katika **1 Wakorintho 14:33, 40** Biblia inasema: **“33 Kwa maana Mungu si Mungu wa machafuko, bali wa amani; vile vile kama ilivyo katika makanisa yote ya watakatifu.... 40 Lakini mambo yote na yatendeke kwa uzuri na kwa utaratibu.”**

Moja kati ya matukio makubwa katik Biblia yanayoonesha jinsi ambavyo Roho wa Mungu huwajia wanadamu ni wakati Yesu anabatizwa **Mathayo 3:16, 17** tunasoma maneno haya: **“16 Naye Yesu alipokwisha kubatizwa mara akapanda kutoka majini; na tazama, mbingu zikamfunukia, akamwona Roho wa Mungu akishuka kama hua, akija juu yake; 17 na tazama, sauti kutoka mbinguni ikisema, Huyu ni Mwanangu, mpendwa wangu, ninayependezwa naye.”** sasa ninaamini kabisa kwamba katika historia ya dunia hii Yesu ni miongoni mwa watu waliompokea Roho Mtakatifu, lakini baada ya kumpokea hakuanza kucheza na kupiga makofi, wala hakuna mahali ambapo Yesu wetu alifanya hivyo ktk Biblia, na bado Biblia inaonesha Yesu alipokea uwezo wa kumpokea na Roho Mtakatifu ambaye yeyote anaweza kumpokea.

Tukio jingine makini sana linaloonesha jinsi watu walivyompokea Roho Mtakatifu ni siku ile ya Pentekoste. Inaelezwa hivi katika maandiko **Matendo 2:2-4**: **“2 Kukaja ghafula toka mbinguni uvumi kama uvumi wa upepo wa nguvu ukienda kasi, ukajaza nyumba yote waliyokuwa wameketi 3 Kukawatokea ndimi zilizogawanyikana, kama ndimi za moto uliowakalia kila mmoja wao...”**

Hili ni moja kati ya matukio makubwa sana katika Kanisa. Ingawa hawa mitume walipokea uwezo wa Roho Mtakatifu, hatuna kumbukumbu ya kucheza kwa step na kuruka, na makelele na maneno yasiyo eleweka huku watu waliopembeni wakiwapigia makofi. Mambo kama hayo kamwe hayakuwahi kutokea katika Biblia. Badala yake kile tunachokiona ni jinsi hawa wanafunzi wa yesu walivyopokea uwezo wa kwenda kuhubiri injili ya Yesu Kristo, na kwa kweli walilihubiri neno la Mungu kwa nguvu sana kiasi kwamba maelfu walitoa maisha yao kwa Mungu na wakaja wakiuliza Ndugu zetu imetupasa kufanya nini? Lakini hapa kuna mmoja anayeuliza kwamba je siku ile walinena kwa lugha? Jibu ni ndiyo, walinena kwa lugha. Walipokea karama ya kunena kwa lugha lakini pia walipokea na karama nyingine pia.

Swali la msingi sana? Kwa nini Mungu awapatie wanadamu karama mbalimbali? Zinakazi gani?

Biblia inatueleza karama nyingine nyingi tu, za Roho Mtakatifu ambazo alizitoa baada ya Yesu kupaa kwenda mbinguni. Katika **Waefeso 4:8, 11, 12** tunasoma: **“8...Hivyo husema, Alipopaa juu aliteka mateka, Akawapa wanadamu vipawa.... 11 Naye alitoa wengine kuwa mitume, na wengine kuwa manabii; na wengine kuwa wainjilisti na wengine kuwa wachungaji na waalimu; ... 12 kwa kusudi la kuwakamilisha watakatifu, hata kazi ya huduma itendeke, hata mwili wa Kristo ujengwe;”**

**Wagalatia 5:22** Lakini tunda la Roho ni upendo, furaha, amani, uvumilivu, utu wema, fadhili, uaminifu, 23 upole, kiasi; juu ya mambo kama hayo hakuna sheria.

**Waefeso 4:8** Hivyo husema, Alipopaa juu aliteka mateka, Akawapa wanadamu vipawa. **11** Naye alitoa wengine kuwa mitume, na wengine kuwa manabii; na wengine kuwa wainjilisti na wengine kuwa wachungaji na waalimu;

**1 Wakorintho 14:26** Basi, ndugu, imekuwaje? Mkutanapo pamoja, kila mmoja ana zaburi, ana fundisho, ana ufunuo, ana lugha, ana tafsiri. Mambo yote na yatendeke kwa kusudi la kujenga.

Roho Mtakatifu hulipatia kanisa karama mbalimbali. Katika **1 Wakorintho 12:28** anasema Paulo: **“28 Na Mungu ameweka wengine katika Kanisa, wa kwanza mitume, wa pili manabii, wa tatu waalimu, kisha miujiza, kisha karama za kuponya wagonjwa, na masaidiano, na maongozi, na aina za lugha.”**

Ukiangalia katika mtiririko, karama ya aina za lugha ni ya mwisho kabisa. Lakini leo hii karama hii ya kunena kwa lugha ndiyo ambayo imeinuliwa juu kuliko karama nyinginezo. Imeaminika na kufundishwa na wengi kwamba kama mtu hajapokea karama ya kunena kwa lugha, basi huyo bado hajaokoka. Wengi wa wahusika wakubwa kabisa katika Biblia hawakupokea karama ya kunena kwa Lugha, na Biblia inatuonesha kwamba kwa hakika wataokolewa. Wala hatuna kumbukumbu yoyote kwamba Yesu alinena kwa lugha; ikiwa ingalitokea hivyo basi Biblia ingalituonesha.

Sasa, siku ile wanafunzi waliponena kwa lugha katika siku ya Pentekoste inamaana walizungumza kwa namna ambayo watu wengine hawakuelewa? **Matendo 2:6, 8: "...Basi sauti hii iliposikiwa makutano walikutanika, wakashikwa na fadhaa, kwa kuwa kila mmoja aliwasikia wakisema kwa lugha yake mwenyewe."** Wanafunzi wa Yesu hawakuanza kuunguruma na kupaza sauti katika namna ambayo watu wengine walikuwa hawaelewi, wala hawakuanza kuzungumza katika lugha za ajabu ambazo watu wengine walikuwa hawaelewi, lakini waliongea katika namna ambayo watu wengine walisikia na kuelewa. Watu walikuwa wamekusanyika Yerusalelem, katika hili tukio maalum, kutoka pande mbalimbali za dunia hii, na wanafunzi wa Yesu waliwahubiria kwa lugha mbalimbali. Na watu walasemezana wao kwa wao: **"8 Imekuwa basi sisi kusikia kila mtu lugha yetu tuliyojaliwa nayo?"** Hivyo basi, wanafunzi walizungumza lugha za kueleweka kwa watu wa mataifa mbalimbali.

Shetani amejaribu kuubadili kidogo kila ukweli ambao uko katika Biblia. Na pia amejaribu kuigiza na kupotosha ukweli kuhusu kunena kwa lugha. Hata kama itaonekana kuwa jambo la ajabu, hata waganga wa kienyeji wanaongea katika lugha za ajabu kama hizo hizo zisizoeleweka, sasa hapo utasema ni karama ya Roho wa Mungu au roho wa Shetani? Hawa waabuduo mashetani na watu wa mizimu hupaza sauti zao na kupiga kelele sana, wakisema maneno ambayo wakati mwingine hayaeleweki, wanapiga makofi, na wanaunguruma. Halafu na mdundo wa ngoma unakuwa pembeni hapo, hawana tofauti sana na makanisa mengi ya leo ambayo yamejiita makanisa ya roho.

**Ufunuo 16:13 Nikaona roho tatu za uchafu zilizofanana na vyura, zikitoka katika kinywa cha yule joka, na katika kinywa cha yule mnyama, na katika kinywa cha yule nabii wa uongo. 14 Hizo ndizo roho za mashetani, zifanyazo ishara,**

Hayo yanatokea sehemu nyingi tu duniani. Lakini Paulo anasema: "Mungu wetu si Mungu wa Machafuko." Mungu anasema nini anapooa mambo hayo yakitokea, watu wakidai wana-Roho wa Mungu, na huku wakiishi kinyume na neno linavyosema.

Walio wengi leo hii wamedanganywa na Ibiilisi wakidhani ni uwezo wa Roho Mtakatifu. Mungu anatumieze katika **Matendo 5:32: "Na sisi tu mashahidi wa mambo haya, pamoja na Roho Mtakatifu ambaye Mungu amewapa wote wamtii."** Wengi wa wale wanaodai kwamba wanaye-Roho Mtakatifu wanaivunja amri ya Mungu wazi wazi. Mungu anasema atawapa Roho wake wale wanaomtii na hawa ni wale wanaoshika amri zake Mungu. Ngoja tusome maneno ya Yesu Kristo **Yohana 14:15-17: "15 Mkinipenda, mtazishika amri zangu. 16 Nami nitamwomba Baba, naye atawapa Msaidizi mwingine, ili akae nanyi hata milele;**

Maisha ya mtu yeyote yule ambaye anampenda Mungu kwanza yataonekana kwa jinsi anavyozishika amri za Mungu na huyo ndiye ambaye Biblia inasema atapokea ahadi ya kupewa Roho Mtakatifu.

Katika **Yohana 14:21** Yesu alisema: **"21 Yeye aliye na amri zangu, na kuzishika, yeye ndiye anipendaye; naye anipendaye atapendwa na Baba yangu; nami nitampenda na kujidhihirisha kwake."** Yeyote yule asiye na utayari wa kuzishika amri za Mungu, hawezi vipawa vya Roho wa Mungu. Ukimpenda Mungu kwanza kabisa utatamani umtii katika amri zake kuanzia ya kwanza, ya pili, ya tatu, ya nne, na kuendela

Biblia inasema katika **1 Yohana 5:3: "Kwa maana huku ndiko kumpenda Mungu, kwamba tuzishike amri zake; wala amri zake si nzito.** Mtu anawezaje kusema anampenda Yesu, na kusema ameokoka na hapo hapo bado hataki kuitii amri ya Mungu? Hivi ungaliweza kumzungumzia je motto ambaye anasema anawapenda wazazi wake lakini hataki kuwatii?;

Katika **1 Yohana 2:4** tunaambiwa: **"Yeye asemaye, Nimemjua, wala hazishiki amri zake, ni mwongo, wala kweli haimo ndani yake."** Wengi wetu leo hii wanasema wanampenda Yesu, na kwamba ni Mwokozi wao, na kwamba wameokolewa kwa neema lakini wakati huo huo hawako tayari kumtii Mungu kwa yake anayoyaagiza. Mungu anasema watu kama hao ni waongo. Kumbuka hili kwamba wale ambao hawaitii sheria ya Mungu, hawawezi kuwa rafiki wa Mungu, kwa sababu gani kwa sababu hawajaitii sheria ya Mungu.

**Warumi 8:7 “Kwa kuwa ile nia ya mwili ni uadui juu ya Mungu, kwa maana haitii sheria ya Mungu, wala haiwezi kuitii.”**

Je, Mungu anaweza kumpatia adui yake yaani mtu asiye na utayari wa kumtii karama zitakazotumika kulijenga kanisa lake? Hapana, rafiki, karama ya kunena kwa lugha, karama ya uponyaji, na karama nyingine pia hazitolewi kwa wale ambao wanapingana na ukweli wa Mungu. Wengi wa hao wanaodhani wanakarama za roho wamedanganyika

Labda tujiulize swali kidogo, kwa nini Yesu alituhidi kutupatia Roho Mtakatifu? Ngoja tusome sababu ya msingi kabisa ya kuja kwa Roho Mtakatifu **Yohana 16:13: “Lakini yeye atakapokuja, huyo Roho wa kweli, atawaongoza awatie kwenye kweli yote...”** kumbuka kwamba Roho wa Mungu atatuongoza katika kweli yote.

Lakini tujue ya kwamba Mungu hatawadai chochote baba zetu kwa kile ambacho hawakufahamu. Maana katika **Matendo 17:30** anasema: **“30 Basi, zamani zile za ujinga Mungu alijifanya kama hazioni; bali sasa anawaagiza watu wote wa kila mahali watubu...”** Lakini baada ya kuusikia ukweli na bado usiwe tayari kuufuata Biblia inasema, **Yakobo 4:17: “Basi yeye ajuaye kutenda mema, wala hayatendi, kwake huyo ni dhambi.”**

Hebu tuombe kwa moyo wa dhati ili kwamba Roho wa Mungu atuongoze katika ile kweli yote. Yesu alisema katika **Yohana 14:26: “26 Lakini huyo Msaidizi, huyo Roho Mtakatifu, ambaye Baba atampeleka kwa jina langu, atawafundisha yote, na kuwakumbusha yote niliyowaambia.”** Iko wazi kwamba **Roho wa Mungu atawaongoza wakrito katika kweli yote.** Kabla Yesu hajapaa kwenda mbinguni aliwaambia wanafunzi wake, **Mathayo 28:19, 20: “Basi, enendeni, mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mkiwabatiza kwa jina la Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu; 20 na kuwafundisha kuyashika yote niliyowaamuru ninyi;”** kwa hiyo Roho Mtakatifu hutusaidia kuuelewa ukweli na kutusaidia kuelewa kiasi kwamba tutakwenda kuwaeleza wengine kuyashika yote ambayo Roho wa Mungu.

Katika **Yohana 16:7, 8** Yesu aliwaeleza wanafunzi wake: **“...7 Lakini mimi nawaambia iliyo kweli; yawafaa ninyi mimi niondoke, kwa maana mimi nisipoondoka, huyo Msaidizi hatakuja kwenu; bali mimi nikienda zangu, nitampeleka kwenu. Naye akiisha kuja, huyo atauhakikisha ulimwengu kwa habari ya dhambi, na haki, na hukumu.”** Roho wa Mungu huja na nguvu ya ushawishi. Swali la msingi ni kwamba ni kwa namna gani tunaitikia mwito wake maishani mwetu?

Katika **Matendo 24:25** tunasoma: **“...25 Na Paulo alipokuwa akitoa hoja zake katika habari ya haki, na kuwa na kiasi, na hukumu itakayokuja, *Feliki akafanya hofu akajibu, Sasa enenda zako, nami nikipata nafasi nitakuita.*”** Ndugu zangu na rafiki zangu, tunapousikia ukweli huu na mioyo yetu ikichomwa hebu tusiifanye mioyo yetu kuwa migumu. Tuiseme nitafanya maamuzi kesho, tuiseme naogopa kuteseka, tuiseme nitafukuzwa nyumbani, huyo ni Roho wa Mungu anayetuongoza katika kweli, na vikwazo viwavyo vyote huletwa na yule Ibilisi ili tushindwe kufanya maamuzi ya kumfuata Yesu katika kweli yote anayotuoongoza Roho Mtakatifu

#### **Hatari inayotukabili kwa haraka sana:**

Katika **Waebrania 2:3** Paulo alisema: **“tutaweza je kupona tisipojali wokovu mkuu namna hii...”** Kutokujali! Hebu tuombe Roho wa Mungu atawale katika mioyo Yetu! Naye atatuongoza katika ukweli wote, na kutuoyesha mahali ambapo hatukuwa sahihi, ili kwamba tuwe tuyari kuufuata na kamwe tusirudi tena katika mazoea ya zamani. Tafadhali tusipuuze kweli yoyote ile ambayo tumeisikia, tuingoja kesho tunaweza tukawa tumechelewa sana.

Swali jingine la Muhimu ni kwamba, “kweli ni nini?” Yesu alisema in **Yohana 17:17: “Uwatakase kwa ile kweli. Neno lako ndiyo kweli.”**

Ikiwa Roho wa Mungu atatuongoza katika kweli yote na kweli yake yake ni neno lake na neno lake tunajua ya kwamba ni Biblia, Basi Roho wa Mungu atatusaidia kuielewa na kuifuata kweli ya Biblia. Nimewasikia watu wakisema, “ndiyo, hiyo ni Biblia, ila mimi naenda kwanza nyumbani kumuomba Roho Mtakatifu.” Niwaeleze tu kwamba Roho wa Mungu hatakuonesha kitu ambacho kipo kinyume na Biblia, atakuongoza katika kweli yote ya Biblia.

Yeye ndiye mwasisi wa Biblia na hawezi kujichanganya hata kidogo. Katika 2 Petro 1:21 tunasoma: “Maana unabii haukuletwa po pote kwa mapenzi ya mwanadamu; bali wanadamu walinena yaliyotoka kwa Mungu, wakiongozwa na Roho Mtakatifu.”

**KIELELEZO:** Mama mmoja alikwenda kuomba Mungu amuoneshe, na wakati akiomba alisema ameona neno “Jumapili” kwa maandishi kama ya moto, na akashawshika kwamba hiyo ndiyo iliyokuwa siku sahihi kama sabato. Aliukataa ukweli wa Mungu na akamuhuzunisha Roho wa Mungu. Kwa kuwa Roho wa Mungu ndiye aliyeongoza uandishi wa Biblia angekuwa Yeye angemuongoza katika kweli ya neno lake.

Ni kupitia Roho Mtakatifu na neno lake tunajua yale tunayokosea. Katika **Waebrania 4:12** anasema: “**Maana Neno la Mungu li hai, tena lina nguvu, tena lina ukali kuliko upanga uwao wote ukatao kuwili... tena lachoma hata kuzigawanya nafsi na roho, na viungo na mafuta yaliyomo ndani yake; tena li jepesi kuyatambua mawazo na makusudi ya moyo.**”

Hatutakiwi kuugeuzia kisogo ukweli wa neno la Mungu na kuifanya mioyo yetu migumu pale Roho wa Mungu anapotusihia. Nimewasikia watu wakisema tunaenda nyumbani kuombea suala la Ubatizo tuone Roho wa Mungu anasemaje, hauhitaji kumuuliza Mungu kile ambacho tayari amekwisha kukisema moja kwa moja katika neno lake. Tunapofanya hivyo ni kama tunamtia Mungu majaribuni na tunajitia majiribu na katika hatari ya kufuata udanganyifu. Kwa maana tunasoma **2 Wathalonike 2:11, 12: “Kwa hiyo Mungu awaletea nguvu ya upotevu, wauamini uongo;... ili wahukumiwe wote ambao hawakuiamini kweli, bali walikuwa wakijifurahisha katika udhalimu.”** Hii inaonesha waziwazi kabisa kwamba kama tukiukataa ukweli tutaishi kwa kadri ya giza

Ndugu zangu, je, unaongozwa na Roho wa Mungu? Katika **Warumi 8:14** anasema: “**Kwa kuwa wote wanaoongozwa na Roho wa Mungu, hao ndio wana wa Mungu.**” ikiwa Roho anakuongoza basi utafanya maauzi ya kutembea katika nuru Mara moja pale kweli inapofunuliwa kwako. Hautasita mara tu unapoutambua ukweli maana tayari umefanyika kuwa mwana wa Mungu.

#### **Roho wa Mungu hataendela kutusubiri milele na milele**

Katika **Mwanzo 6:3 Mungu alimwambia Nuhu: “Bwana akasema, Roho yangu haitashindana na mwanadamu milele...”** wpendwa ni lazima tuelewe kwamba Roho wa Mungu hatashindana na sisi pia milele. Kuna saa itafika Roho atatuacha nasi tutakuwa tumetenda dhambi ya kumkufuru

Katika **Yohana 6:44** Yesu alisema: “**Hakuna mtu awezaye kuja kwangu, asipovutwa na Baba aliyenipeleka; nami nitamfufua siku ya mwisho.**”

Mungu Baba anatumvuta kupitia Roho Mtakatifu. Hatuji kwa Mungu pale tunapotaka sisi, lakini tunakuja pale Roho wa Mungu anapotuvuta. Tunapokataa kuvutwa kwake, na kuifanya mioyo yetu kuwa migumu, tunamuhuzunisha Roho wa Mungu. nasi tunapompokea Roho Mtakatifu na kuukubali wito wake, atatuongoza katika maisha matakatifu siku hata siku

Kuna watu wanasema haijalishi mtu anavyoishi au anavyotenda, alimradi tu wanadai kuwa wakristo basi hiyo imetoshwa. **Yakobo 2:19, 20: “Wewe waamini ya kuwa Mungu ni mmoja; watenda vema. Mashetani nao waamini na kutetemeka! Lakini wataka kujua, wewe mwanadamu usiye kitu, kwamba imani pasipo matendo haizai?”** Kwa hiyo basi haijalishi tunakiri sisi ni wakristo lamuhimu ni kufanya yale ambayo Mungu ameagiza tuyafanye.

Je umewahi kuisikia sauti le ya upole ikikuita? Watuwengine wameiita DHAMIRA. Katika **Isaya 30:21 “na masikio yako yatasikia neno nyuma yako, likisema, Njia ni hii, ifuateni; mgeukapo kwenda mkono wa kulia, na mgeukapo kwenda mkono wa kushoto.”**

Najua na ninao uhakika wapo watu hapa ambao wanaisikia sauti ya namna hiyo ikinong’ona mioyoni mwao. Taafhdali usisite wala usikatae huyo ni Roho wa Mungu kabisa anayekuongoza kufanya maamuzi ya kumfuata Mungu... acha kusita tafadhali fanya maamuzi jioni ya leo. Tunapo isikia sauti hii ya Roho Mtakatifu ikitushawishi kufanya maamuzi na kusikia sauti ikisema njia ni hii ifuate. Usiufanye moyo wako kuwa mgumu maana kuna saa sauti hiyo itakoma na kamwe haitasikika tena.

Mungu atakusamehe dhambi zote ulizowahi kufanya, anasema katika **Yohana 6:37: “...37 Wote anipao Baba watakuja kwangu; wala ye yote ajaye kwangu sitamtupa nje kamwe.”** Wote watakao mjia Mungu Biblia inasema Mungu hatamtupa, mtu aliyendani ya hatari ni yule ambaye anaisikia sauti ya Mungu lakini hataki kufanya maamuzi ya kuja. Huyo atakuwa na dhambi isiyosameheka, maana kama haji atasamehewaje? Kama hatasamehewa maana yake atapotea milele... Kama ukielewa sabato, na ukasikia moyoni mwako njia ni hii ifuate, nab ado usiwe tayari kuifuata... Dhambi hiyo haitasamehewa maana haukuja kuiungama, na mwisho wa siku, kuna saa itafika hautaisikia tena ile sauti ya onyo. Ni vema leo ukaungama na kuja kwa Yesu leo, wala si kesho.

**Musa alisamehewa dhambi ya mauaji**, Paulo mtesaji alisamehewa, Yakobo mdanganyifu alisamehewa dhambi ya kumdanganya baba yake na kumuibia ndugu yake. Petro alimkana Yesu vikali kabisa lakini alisamehewa. Dhambi zote hizi zilisamehewa na wakafanyika kuwa watoto wa Mungu. kwa nini? Kwa sababu waliisikia sauti ya Mungu ikizungumza nao kwa sauti ya upole kabisa na kuwaongoza katika kufanya toba.

Daudi alikua amefanya dhambi kubwa kabisa mbele za Mungu lakini alipomlilia Mungu katika Zaburi Mungu alimsikia, Zaburi 51:10 “Ee Mungu, uniumbie moyo safi, Uifanye upya roho iliyotulia ndani yangu.” Daudi alikuwa ametenda dhambi ya uzinzi na alikuwa ametenda dhambi ya uuaji pia, kwa kuwa Mungu ni wa rehema sana na upendo mwingi, alimhurumia akamsamehe dhambi zake.

**Mithali 16:25** inasema: **“Iko njia ionekanayo kuwa sawa machoni pa mtu; Lakini mwisho wake ni njia za mauti..”** Wahalifu wengi sana leo hii wanajaribu kuhlalisha maovu yao. Hata hivyo leo hii imekuwa jambo la nadra sana kusikia mtu akikiri udhaifu na maovu yake. Leo hii ni rahisi sana mtu kuendelea kuishi katika maovu hasa pale anapojiwekea msimamo kwamba yu sahihi. Mara ya kwanza anapoanza kufanya hivyo anajisikia huzuni sana, lakini kadri anavyorudia rudia, anaendelea kuona hali hii ni ya kawaida kabisa siku hata sikua. Huyo anakuwa amemhuzunisha Roho Mtakatifu.

Kutakuwa na wengi sana ambao watakuwa wamefanya dhambi ya kumkufuru Roho Mtakatifu bila kujua siku ile atakapokuja. Katika **Mathayo 7:22, 23 we read: “22 Wengi wataniambia siku ile, Bwana, Bwana, hatukufanya unabii kwa jina lako, na kwa jina lako kutoa pepo, na kwa jina lako kufanya miujiza mingi? ... 23 Ndipo nitawaambia dhahiri, Sikuwajua ninyi kamwe; ondokeni kwangu, ninyi mtendao maovu!**

Huu ni ushahidi wa kutosha kutuonesha kwamba wengi wetu leo hii wako makanisani wakidhani kwamba wako sahihi sana. Lakini wapo leo wengi wanaoishi katika uzinzi, uongo, na kwa kweli wengi wetu leo hii makanisani wanivunja amri ya kuishika Sabato. Kuna wengi ambao wanamigogoro na ndugu zao na wameshikilia moyo wa kinyongo Siku Yesu akija atawaambia ondokeni kwangu ninyi mtendao maovu.

Mungu anakuwa na anakupenda sana, na sauti unayoisikia ni saiti ya Roho Mtakatifu, tafadhali itika.

Wito na ombi